



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BARIADI
Telegrams "MAJI Tel No: 028-2700204 S.L.P 64, Bariadi
Fax: 028-2700204, Barua pepe: md@baruwasa.go.tz



MKATABA MDOGO WA AJIRA ZA MAFUNDI
KATI YA
MKURUGENZI MTENDAJI WA BARUWASA S.L.P 64, BARIADI, SIMIYU

NA

KAZUKI JOHN KAYANDA, S.L.P 526, BARIADI

KWA

KAZI YA UFUNDI WA KUJENGA MTANDAO WA MAJI BARIADI MJINI

MKATABA NA.BRD/UWASA/2021-2022/W/UCH/02

Novemba, 2021

FOMU F2: MKATABA MDOGO WA AJIRA ZA MAFUNDI

KAZI YA UFUNDI WA KUJENGA MTANDAO WA MAJI BARIADI MJINI

MKATABA HUU unafanyika leo tarehe 23 mwezi Novemba, 2021.....

BAINA YA

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BARIADI (BARUWASA)
S.L.P 64 (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri au BARUWASA") kwa upande mmoja;

NA

Kazuki John Kayanda S.L.P 526 BARIADI (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiriwa au Fundi") kwa upande mwingine.

KWAMBA kwa pamoja Mwajiri na Mwajiriwa watajulikana kama pande mbili za Mkataba.

AMBAPO:

- a) Mwajiri ni Mamlaka ya maji wenye jukumu la kutekeleza ujenzi wa miradi ya maji mjini na kusimamia utoaji wa huduma ya maji na usafi wa mazingira mjini.
- b) Mwajiriwa ni mtu binafsi anayefanya shughuli zake binafsi za ujenzi **Bariadi**;
- c) Mwajiri anakusudia kumwajiri Mwajiriwa kwa kipindi cha muda mfupi wa miezi miwili;
- d) Mwajiriwa anakubali matakwa ya Mwajiri na anakubali kwa hiari yake mwenyewe kuajiriwa kwa muda mfupi kama fundi bomba wa kuchimba, kulaza na kufukia bomba

MKATABA HUU UNASHUHUDIA kwa pande zote mbili kukubaliana kama ifuatavyo:

1. MADHUMUNI YA MKATABA

Mkataba huu ni kwa ajili ya kazi ya kujenga mtandao wa mabomba ya kusambaza maji katika mji wa Bariadi.

Mchanganuo wa kazi zitakazofanyika ni kama ifuatavyo;

- ❖ Kuchimba mitaro yenye urefu wa mita 8,500 kwa ajili ya kulaza mabomba ya kusafirisha maji kutoka kisimani kwenda kwenye tanki pamoja na mabomba ya usambazaji maji.
- ❖ Kulaza mabomba, kuunga bomba kwa bomba na viungio vyake pamoja na kufukia mitaro.
- ❖ Kujenga chemba nane (08) kwa ajili ya 'gate Valves', Air Valves, Bulk Meters
- ❖ Kujenga nguzo nane (08) za kushikilia mabomba kwenye mwinuko, na miamba
- ❖ Kuweka alama 'marker posts' (170) maeneo yote ambayo mabomba yatapita.
- ❖ Kujenga sehemu za kuchanganyia dawa (installation of simple chlorination unit)
- ❖ Kuweka "bulk meter" kwenye tank na kwenye bomba la kusambaza maji

2. MUDA WA UTEKELEZAJI WA KAZI

Kazi hii itafanyika kwa muda wa siku 30, ambapo itaanza tarehe 23/11/2021 na itakamilika tarehe 23/04/2022

3. MALIPO YA UTEKELEZAJI WA KAZI

- a) Mwajiriwa atalipwa jumla ya kiasi cha Tshs **42,350,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu;
- b) Malipo ya Mwajiriwa yatakuwa ni fedha za kitanzania tu (*Tanzanian Shillings*);
- c) Malipo hayo yatalipwa aidha kwa fedha taslimu au hundi ambayo italipwa benki;
- d) Malipo ya Mwajiriwa yatalipwa kwa awamu tatu (3) kama ifuatavyo:
 - i. Malipo ya awali yatakuwa kiasi cha Tsh. **8,470,00/=** ambapo ni sawa na asilimia 20 ya kazi .
 - ii. Malipo ya awamu ya Pili yatakuwa kiasi cha sh **21,175,000/=** ambayo yatalipwa mara baada ya kukamilisha asilimia 50% ya kazi yote.
 - iii. Malipo ya awamu ya Tatu na ya mwisho yatakuwa kiasi cha Tsh. **12,705,000/=** ambayo yatalipwa mara baada ya kukamilisha kazi yote kama ilivyoainishwa kwenye mkataba.
- e) Kabla ya malipo ya mwisho kufanyika, Mwajiriwa anapaswa kuwasilisha taarifa zote zinazohitajika na kufanya marejesho ya vifaa vyote vya kazi na fedha za mradi kama zitakuwepo.

Masharti mahsusi ya nyongeza kuhusiana na utekelezaji wa mradi huu ni pamoja na:

- a) Mvua kuzidi kunyesha na kusababisha kushindwa kuingia eneo la kazi
- b) Kucheleweshwa vitendea kazi (construction materials)
- c) Kuchelewa kwa Malipo

KWA USHUHUDA HUU, pande zote mbili zinaweka sahihi zao katika Mkataba huu siku na tarehe kama ilivyooneshwa hapa chini:

MWAJIRI (BARUWASA)

Jina:

Sahihi:

Cheo:

Tarehe:

Mwaliya Masafu
[Signature]

MKURUGENZI MTENDAJI
MILAKAYA MAJI NA USAFI WA
KAZINGIRA
S.L.P. 64
BARIADI

Shahidi:

Jina:

Sahihi:

Cheo:

Tarehe:

Chadwick W. Mbunde
[Signature]
Meneja Ufundi
23/11/2021

MWAJIRIWA (FUNDI)

Jina:

Sahihi:

Cheo:

Tarehe:

KAZUKI JOHN KAYANDA
[Signature]
KAZUKI J. KAYANDA
S.L.P. 526
BARIADI
FUNDI TAR

Shahidi:

Jina:

Sahihi:

Cheo:

Tarehe:

ELISITA ISAAC MARIKA
[Signature]
CO
23/11/2021